KISWAHILI KARATASI 2

KAGONDO SECONDARY SCHOOL

KCSE Post Trial Exam

Lugha

September 2015

Saa 2½

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yafuatayo**

Kwa kipindi cha miezi kadha iliyopita tumeshuhudia vyombo vya dola vikitia makali yake kwenye upekuzi na hata kupiga doria usiku na mchana katika jitihada za kulinda nchi.Mpango huu ni kweli umeonekana kufanya kazi hivi kwamba hata magaidi wenyewe wameshindwa kupenya katika miji na sasa kuhiari kijinga kushambulia magari ya abiria kitendo ambacho ni cha kuonyesha uwoga. Kwa hatua hiyo, navipa vyombo vya dola kongole. Jambo ambalo lafaa kujulikana ni kwamba mikakati ya kulinda nchi haifai kuwa ni ya wakati mmoja tu, mbali inafaa kuwa ni zoezi la kila siku. Magaidi nao huwa macho huku yakijua bayana kwamba wakati wa kulala kwa walinzi unapokuwepo, basi wanapata nafasi ya kututupia 'viazi' ukipenda grunedi.

Kama ilivyo kawaida katika mataifa mengi barani Afrika, ni bayana kwamba bado kungali na mianya mingi ambayo magaidi wa kimataifa huendelea kutumia. Dosari bado zipo. Kwa mfano mipaka mingi ya nchi hizi huwa kama lango kuu la ugaidi wa kimataifa, kwani kuenea kwa saratani ya ufisadi halimo tu maofisini mbali pia kwenye mipaka yetu.

Kama kupata kitambulisho, pasipoti na stakabadhi zingine za kusafiri nchini Kenya ashakum si matusi ziligeuzwa 'maandazi' ya kariakoo basi niambie ni nani hawezi kuingia na kutoka nchini bila usumbufu wowote ule bora tu anayehitaji ana hela mkononi? Kwa kuikubali hongo kuwa ufunguo wa kila kitu, Wakenya wenzangu hapo naona ni kama tumejiweka kwenye kikaango kilicho juu ya moto mkali. Hapa hakuna aliye na bahati, tajiri kwa masikini wamo kwenye mtego huu hatari. Kwa mtindo ambao tunafuata wa kutoa ajira katika idara mbalimbali za ulinzi, inabidi serikali iwe na uangalifu sana hasa kwenye suala nzima la kuhakikisha stakabadhi wanazohitaji si ghushi.

Pasina kufanya hivyo hapo tena tunaweza kuwapata maadui wanaopenya na kujifanya walinzi wetu kumbe ni majasusi wa magaidi. Kila Mkenya anafaa kujihisi kulindwa. Miji, vijiji na hata vitongoji vinafaa kuwa na usalama wa kutosha, kwani kila Mkenya ni mlipa ushuru na hatufai kuona labda tabaka la juu likipendelewa huku mitaa ya mabanda ikiachiwa mbwa koko kama walinzi wao.

Suala lingine muhimu ni kuangaziwa upya usalama kwenye magari ya usafiri. Juzi tulishuhudia mabasi mawili yakilipuliwa kwenye barabara ya Thika huku tukijua fika kwamba, mpango walinda nchi ungalipo.La kusitikitisha ni kuona kwamba, madereva na utingo wao walikamatwa na kufunguliwa

mashtaka kwa kutozuia shambulizo hilo.  Je, hii ni sheria gani?  Dereva ataendesha gari au atachukua jukumu la walinda usalama?  Waswahili walinena kwamba mkubwa ni jaa na kwa hivyo Rais wa taifa ndiye anayefaa kubeba mzigo mzima wa usalama wetu bila kubananga wasaa.  Wengine ambao wanafaa kuwajibika ni wakuu wote wa idara mbalimbali za usalama.

Usalama wako na wangu ni muhimu, elewa bayana kwamba bila usalama watalii hawawezi kuja kututembelea. Bila ya usalama maendeleo ya taifa kamwe hayawezi kupatikana, ndiposa kila jitihada sharti zifanywe ili wote waweze kuendelea kuyafurahia matunda ya uhuru wetu.Ada ya mja kunena muungwana ni vitendo,  hatufai tu kuimba wimbo wa Linda nchi, ilhali mabasi barabarani hayana usalama.  Hebu na tuuone ulinzi endelevu na hapo tutawakomoa magaidi kwa yakini.

**Maswali**

1.***Ipe taarifa*** hii anwani mwafaka. (Al 1)

2. ***Kwa nini magaidi*** wanashambulia magari ya abiria? (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

3. ***Eleza njia tatu*** ambazo zinatumiwa na magaidi kutekeleza unyama wao. (Al 3)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

4. ***Ni njia gani*** ambazo magadii hutumia kuingia nchi wanazoazimia kutekeleza uhalifu?

(Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

5. ***Kwa nini*** suala la usalama kwenye magari ya usafiri ni muhimu? (Al 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

6. ***Ni njia zipi*** zinazoweza kutumiwa kupunguza mashambulizi ya kigaidi kulingana na mwandishi? (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

7. ***Eleza athari*** za utovu wa usalama. (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

8. ***Eleza*** neno au mafungu ya maneno kama yalivyotumiwa katika kifungu. (Al 2)

(a) Vyombo vya dola

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(b) Jaa

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata*.**

Tume ya kutathmini mishahara (SRC) inafaa kuchunguza kwa makini pendekezo lake la kutaka umri wa kustaafu kwa watumishi wa umma upunguzwe kutoka miaka 60 hadi 55.

Kulingana na SRC, kupunguzwa kwa umri wa kustaafu kutasaidia kupunguza mzigo mzito wa mishahara ambayo hupewa wafanyakazi wa umma na kuacha kiasi kidogo tu cha fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kufanya hivyo ni sawa na kukata mguu kwa sababu una kidonda kabla ya kuutafutia matibabu.

Ikumbukwe kuwa, umri wa kustaafu kwa watumishi wa umma humu nchini uliongezwa miaka mitano iliyopita kutoka miaka 55 hadi 60 baada ya serikali kung'amua kuwa zaidi ya wafanyikazi 20,000 wa umma na walimu walitaka kulipwa pensheni, hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa serikali.

Wakati mjadala wa kutaka kupunguza mishahara minono ambayo watumishi wa umma wanapokea na kuacha masazo kwa ajili ya maendeleo kuzuka mwezi Machi, mwaka huu, Rais, naibu wake pamoja na baraza la mawaziri walitangaza mishahara yao ipunguzwe. Rais pia aliwashinikiza wakuu wa mashirika ya umma kufuata nyayo la sivyo wapigwe kalamu nyekundu.

Mathalani, wasomi wa masuala ya uchumi nchini China, ambapo umri wa wastani wa kustaafu ni miaka 53, wanajikuna kichwa sasa ili kutafuta mikakati ya kuongeza umri huo hadi mika 65 katika kipindi cha miongo miwili ijayo kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kuwalipa wanaostaafu pensheni zao.

Wasomi wa uchumi nchini humo wanadai kuwa pengo lililopo, baina ya umri wa kustaafu wa miaka 53 na wastani wa umri ambao Wachina wanastahili kuishi wa mika 75, ni kubwa mno hivyo kuongeza uwezekano wa mtu kuendelea kuchuka malipo ya baada ya kustaafu kwa zaidi ya miaka 10. Kwa mujibu wa wanauchumi, hali hiyo imesababisha msongamano mkubwa katika hazina ya malipo ya uzeeni. Suala hilo lilisababisha serikali kualika mashirika mbalimbali duaniani yakiwemo Benki ya Dunia na Shirika la Wafanyakazi Ulimwengu (ILO) kutoa mapendekezo yao kuhusiana na hali hiyo.

Benki ya Dunia ilishauri China kuongeza umri wa kustaafu ili kupunguza kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kulipa waliostaafu malipo ya baada ya uzeeni. Nchini Uturuki, mtu anatakiwa kustaafu baada ya kufanya kazi kwa kipindi cha miaka 25. Hiyo inamaanisha kuwa mtu akianza kufanya kazi akiwa na umri wa miaka 20 atatakiwa kustaafu anapotimiza miaka 45.

Hata hivyo, hatua hii ya kustaafisha watu mapema, imekuwa na athari chungu nzima kiuchumi nchini humo huku ikikadiriwa kuwa kufikia mwaka wa 2045 taifa hilo litakuwa linatumia asilimia 6 ya mapato yake kulipa pensheni, endapo mambo hayatabadilishwa.

Hayo ni mataifa machache kati ya mengi ambayo yamejaribu kupunguza umri wa kustaafu na kujutia baadaye. Serikali inafaa kutafuta njia mbadala kukabiliana na tatizo hilo na wala sio kuwaachisha kazi mapema wafanyakazi.

***Maswali***

(a) Kwa maneno yasiyozidi 50, eleza sababu za kuongeza umri wa kustaafu kutoka miaka 55 hadi 60 na athari zake. (Al 7)

***Matayarisho/maadalizi***

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

***Jibu***

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Kwa maneno yako mwenyewe ***fupisha aya tatu za mwisho***. Tumia maneno 70. (Al 8)

***Matayarisho***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

***Jibu***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a. ***Taja*** sifa mbili za mofimu (Al 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

b. ***Tambua*** aina ya viambishi katika: Wanaolimiwa. (AL 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

c. ***Onyesha*** uhusiano wa ngeli ya Ki/Vi na Li-ya (Al 2)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

d. ***Tunga*** sentensi ukitumia vivumishi viashiria radidi vya wastani katika ngeli ya 1-Z1. (Al 2)

………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

e. ***Andika*** katika usemi wa ripoti "*Mbona unamfanyia mwenzako mzaha? Je, utaenda kumwomba msasamaha?"*. Gikundi alimuuliza Zablon (Al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

f. ***Ainisha aina nne*** za vielezi katika sentensi ifuatayo. Mwanafunzi ni yule asomaye vizuri sana kila siku shuleni (Al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

g. ***Andika upya*** sentensi ifuatayo ukibadilisha neno lililopigwa mstari kuwa nomino.

Mkulima alimlimia jirani shamba vizuri mpaka maisha ya jirani huyu yalibadilika (Al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

h. ***Onyesha shamirisho*** na chagizo katika sentensi hii. Lemayan atasafiria basi ili kwenda kumlimia babake shamba kesho jioni. (Al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

i. ***Bainisha viwakilishi*** viambata katika sentensi hizi. Mimi nitawasaidia yeye siwasaidii wengine

(Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

j. ***Nyambua*** katika kauli ya kutendesha. (Al 2)

Kana

……………………………………………………………………………………………………

Ogopa

……………………………………………………………………………………………………

k. ***Kanusha*** katika wingi, Uliko ndiko kuliko nayo (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

l. ***Eleza dhana*** ya:- (Al 2)

a. Silabi

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b. Kiambishi (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

m.***Tumia kitenzi*** soma katika sentensi kama:

Kishazi huru na tegemezi (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

n. ***Changanua*** sentensi kwa mtindo wa matawi.

Kioo kikubwa lilivunjika jana (AL 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

o. ***Tunga sentensi moja*** ukitumia kivumishi cha a- unganifu (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

p. ***Tunga sentensi*** ukitumia kihusishi " *Katika*" kutoa dhana ya hali (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

q. ***Tunga sentensi mbili*** kuonyesha matumizi mawili ya "*Ku*" (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

r. ***Tunga sentensi mbili*** kuonyesha maana mbili ya neno '*ila*' (Al 2)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

s. Taja sauti Mbili za menoni na mbili za kakaa laini (Al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMU JAMII**

*Eleza maana ya istilahi zifuatazo* *(Al 4)*

a) Viziada vya lugha

…………………………………………………………………………………………………………

b) Uwingi lugha

…………………………………………………………………………………………………………

c) Lafudhi

…………………………………………………………………………………………………………

d) Krioli